

**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUTIAMA**

**namba za simu:** **Mkuu wa shule: 0747 656 272** **M/mkuu wa shule: 0763 358 923** **shule ya sekondari kiabakari, S.L.P 637, Musoma.**  
**12/12/2020.**

**JINA LA MWANAFUNZI.....**

**YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA KUTWA YA SEKONDARI KIABAKARI - 2021.**

1. Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Kiabakari mwaka 2021 Shule ya Sekondari Kiabarika ipo umbali wa KM 11 kutoka makao makuu ya Halmashauri ya wilaya ya Butiama. Shule ni ya kutwa (day school) na ni ya wanafunzi mchanganyiko yaani wavulana na wasichana. Mhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021. Aidha Unatakiwa kuripoti shule kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 16/01/2021.

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**A. SARE ZA SHULE; WAVULANA**

- Suruali rangi ya damu ya mzee na nyeusi
- Shati mikono mifupi rangi nyeupe pamoja na tai rangi nyeusi na damu ya mzee
- T-shirt rangi ya njano
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba na soksi nyeusi na si vinginevyo

**WASICHANA**

- Sketi rangi ya damu ya mzee na nyeusi zinazovuka magoti.
- Shati mikono mifupi rangi nyeupe pamoja na tai nyeusi na damu ya mzee.
- Viatu vyeusi vya kufunga na kamba na soksi nyeupe na si vinginevyo.

**➤ MAHITAJI MENGINE MUHIMU**

- **Daftari zisizopungua 10 (Counter Books au za kawaida), mathematical set, kalamu, rula.**

**NB: Inashauriwa mwanafunzi awe na sare ya shule pea mbili.**

**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 kama ilivyorekebishwa na sheria na 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu yenye dhamana ya Elimu chini ya ofisi ya waziri mkuu – **TAMISEMI** yenye jukumu la kusimamia na kuendesha elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shulen. Nakala ya sheria za shule imeambatanishwa.

- A. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, pamoja na wanafunzi wengine ni jambo la lazima
- B. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli zote za nje na darasani kulingana na ratiba ya shule ni jambo la lazima
- C. Kushiriki vizuri kufanya maandalizi ya jioni (preparation) inapotakiwa
- D. Kuwahi katika shughuli zote za shulen na zingine utakazopewa.
- E. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- F. Kutunza usafi wa mazingira ya shule na mazingira binafsi ya mwili.
- G. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- H. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- I. Kutunza mali za umma.
- J. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kutunza siha na usafi wake binafsi.
- K. Makoti, vibandiko, vizibao, kofia, kandambili, viatu vya wazi, mikanda mipana na yenye mapambo, haviruhusiwi kamwe kuvaliwa wakati mwanafunzi awapo ndani ya vazi la shule.
- L. Uharibifu wa miundombinu ya majengo, mfano kupasua vioo, kuchafua kuta kwa kuchora au kuandika maandishi yoyote, **Utawajibika kuirudisha katika hali yake ya awali.**

### **3. MAKOSA YAFUATAYO YATAMFANYA MWANAFUNZI KUSIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE KABISA.**

- 1. Wizi ndani au nje ya mazingira ya shule
- 2. Uasherati na Ushoga
- 3. Ubakaji
- 4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyta kama vile Bangi, Cocaine, heroin n.k
- 5. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote.
- 6. Kutoa lugha cha chafu kwa wanafunzi wenzako, walimu na walezi na jamii kwa ujumla.
- 7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- 8. Kudharau bendera ya taifa
- 9. Kuoa na kuolewa
- 10. Kupata/kusababisha/ au kutoa mimba
- 11. Kugoma, kuchochaea mgomo au kushiriki katika mgomo na matendo mengine ya uhalifu.
- 12. Kuvuruga amani na usalama wa shule.
- 13. Kukataa adhabu.
- 14. Kumiliki/kukutwa/kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
- 15. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa.
- 16. Kusuka nywele, kufuga ndevu/nywele/kucha
- 17. Uvaaji wa suruali za kubana (modo)

18. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu nk
19. Kutembelea majumba ya sterehe na nyumba za kulala wageni

#### **4. MATIBABU**

Shule haitoi huduma ya matibabu kwa wanafunzi, hivyo gharama za matibabu ni jukumu la mzazi/mlezi wa mwanafunzi mwenyewe. Shule itatoa huduma ya kwanza tu kwa matatizo ya dharura

Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na mwanafunzi na kuwasilishwa shuleni mara tu baada ya kuripoti ni haya yafuatayo;

- A. Medical Examinaton form ambayo itajazwa na mgaga mkuu wa hospital ya serikali.
- B. Fomu ya maelezo binafsi na historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika vitendo vinavyokwenda kinyume na kanuni na taratibu au sheria za shule.
- C. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria za shule, na maelekezo mengine yatakayotolewa shuleni.

***NB: Fomu hizi zote zitakabidhiwa kwa msajili wa wanafunzi mara tu baada ya Kuripoti shuleni zikiwa zimejazwa vizuri .***

Mwisho, nakutakia maandalizi mema ya kijiungu na shule ya sekondari Kiabakari.

**Karibu sana katika shule ya sekondari kiabakari .**

**NATHAN VEGULA  
MKUU WA SHULE YA SEKONDARI KIABAKARI**

BUTIAMA DISTRICT COUNCIL  
KIABAKARI SECONDARY SCHOOL,  
P. O. BOX 637,  
MUSOMA.

DATE.....

To Medical Officer,

.....  
.....  
.....

Ref:..... (*name of student*)

Please examine the above named student as per medical examination from below:

.....

**HEADMASTER**

**MEDICAL EXAMINATION FOR**

(*To be completed by government medical officer*)

Full name.....

Age..... Height.....(cm) Weight.....(kg)

1. Blood count.....
2. Stool examination.....
3. Urinary.....
4. STDs and other V.D.....
5. T.B and leprosy test.....
6. Eye test.....
7. Ear test.....
8. Chest .....
9. Abdomen.....
10. Spleen.....

Any additional information e.g. Physical impairment, infections, chronic or family diseases (like sickle cell) .....

.....  
.....

I have examined the above named student and I certify that he/she is **FIT/NOT FIT** to pursue secondary education.

.....  
.....  
Signature and official stamp

.....  
.....  
Date

Station.....

.....  
.....  
Designation.....